**Na Mheshimiwa Alice Wahome, EGH**
Waziri
Wizara ya Ardhi, Kazi za Umma, Nyumba na Maendeleo ya Miji ya Jamhuri ya Kenya

# Kenya katika Kikao cha 13 cha Jukwaa la Miji Duniani (World Urban Forum):

***Kuendeleza Masuluhisho ya Makao Kimataifa na Kuimarisha Ushirikiano kati ya Kenya na Azerbaijan***
***Ajenda ya WUF13: Makao kwa Wote kwa Mustakabali Endelevu (Housing the World for a Sustainable Future)***

Kikao cha 13 cha Jukwaa la Miji Duniani (World Urban Forum, WUF13), kilichofanyika huko Baku, Azerbaijan kutoka tarehe 17 hadi 22 Mei 2026, kiliandaliwa chini ya mada ya "Makao kwa Wote (Housing the World): Jamii na Miji Salama na Thabiti (Safe and Resilient Cities and Communities)." Chini ya maandalizi ya shirika la UN-Habitat, WUF13 lilikuwa Jukwaa kubwa zaidi la Miji Duniani kuwahi kufanyika, lililovutia washiriki zaidi ya 58,000 kutoka nchi 176, ikijumuisha Marais, Mawaziri, viongozi wa miji, washirika wa maendeleo, taasisi za kifedha, mashirika ya asasi za kiraia na wadau wa sekta ya kibinafsi.




WORLD
URBAN
FORUM
THIRTEENTH SESSION
WELCOME TO
WUF13
AZERBAIJAN



Jukwaa hilo liliangazia kushughulikia suala la dharura la kimataifa la makao, ambalo kwa sasa linaathiri karibu watu bilioni tatu duniani kote. Majadiliano hayo yaliangazia kuharakisha utekelezaji wa Ajenda Mpya ya Miji (New Urban Agenda, NUA), kuendeleza mpango wa makao ya bei nafuu, kubadilisha sura ya makazi yasiyo





rasmi, kuimarisha maendeleo ya mijini yanayostahimili mabadiliko ya hali ya anga, kuimarisha mifumo ya ufadhili wa makao na kuimarisha ushirikiano wa kusaidia miji endelevu.

Hatua muhimu ya WUF13 ilikuwa Mkutano wa kwanza wa Viongozi, uliowaleta pamoja Viongozi 27 wa Nchi na Serikali ili kujadili changamoto na fursa za maendeleo ya miji. Jukwaa hilo lilihitimishwa kwa kupitishwa






kwa Wito wa Kuchukua Hatua wa Baku (Baku Call to Action), mfumo wa hoja 15 unaozihimiza serikali na wadau kulipa kipaumbele suala la makao kama haki ya binadamu, kubadilisha mifumo ya ufadhili wa nyumba, kuiwezesha miji na kuharakisha utekelezaji wa ahadi za maendeleo ya kudumu ya miji.

**Mapokezi ya Waziri nchini Azerbaijan**

Kushiriki kwa Kenya katika WUF13 kuliongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. William Samoei Ruto, CGH, pamoja na Waziri Mkuu wa Baraza la Mawaziri Dkt. Musalia Mudavadi, EGH, Waziri wa Ardhi, Kazi za Umma, Nyumba na Maendeleo ya Miji Mheshimiwa Alice Wahome, EGH, na maafisa wengine wakuu wa serikali.

Kwa Mheshimiwa Alice Wahome, kongamano la WUF13 lilitoa jukwaa muhimu la kuonyesha maendeleo ya Kenya katika mpango wa nyumba za bei nafuu, maendeleo ya miji na ustahimilivu wa hali ya anga. Waziri Wahome aliwasilisha Taarifa ya Kitaifa ya Kenya wakati wa Mkutano wa Ngazi ya Juu kuhusu Ajenda Mpya ya Miji na kuongoza sehemu ya kikao kilichotengwa kwa taarifa za kitaifa za Nchi Wanachama. Kupitia majadiliano haya, Kenya iliangazia mbinu zake bunifu za uwezeshaji wa mpango wa nyumba za bei nafuu, mbinu za ufadhili na maendeleo jumuishi ya miji. Waziri pia alishiriki katika majadiliano ya ngazi ya juu kuhusu kubadilisha sura ya makazi yasiyo rasmi, mageuzi ya ufadhili wa makao, hatua za miji za kukabiliana na mabadiliko ya hali ya anga na Mkataba wa Afrika wa Nyumba za Bei Nafuu (Africa Affordable Housing Compact). Majadiliano haya yaliwezesha Kenya kuelezea maarifa yaliyopatikana kutokana na Mpango wa Nyumba za Bei Nafuu, Kujenga Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Hali ya Anga Mijini kupitia mradi wa Urban Poor (Building Climate Resilience with the Urban Poor, BCRUP), na miradi bunifu inayoongozwa na kaunti kama vile Chuka Market Crèche katika Kaunti ya Tharaka Nithi.

Zaidi ya vikao rasmi, WUF13 ilitoa fursa muhimu ya kubadilishana maarifa, kujenga mahusiano na ushirikiano. Kenya iliandaa matukio ya pembeni kwa ufanisi mkuu, ikaonyesha mafanikio yake kupitia Banda la Kenya (Kenya Pavilion) katika Urban Expo, na kushiriki katika mikutano ya pande mbili na washirika wa maendeleo na nchi kadhaa. Fursa hii iliimarisha nafasi ya Kenya ya uongozi inayokua katika kuwa kielelezo




cha mijadala ya kimataifa kuhusu maendeleo ya miji na kuendeleza vipaumbele vya Afrika kuhusu makao na miji endelevu.

**Kuimarisha Mahusiano kati ya Kenya na Azerbaijan katika Sekta ya Nyumba**

Moja ya matokeo muhimu zaidi ya kushiriki kwa Kenya katika WUF13 ilikuwa kuimarika kwa mahusiano kati ya Jamhuri ya Azerbaijan na Jamhuri ya Kenya, katika nyanja ya mipango ya miji na maendeleo ya makao. Wakati wa Jukwaa hilo, Kenya na Azerbaijan zilitia saini Mkataba wa Maelewano (Memorandum of Understanding, MoU) kuhusu Ushirikiano katika Mpango na Maendeleo ya Miji. Makubaliano hayo yalitiwa saini na Mheshimiwa Alice Wahome, Waziri wa Ardhi, Kazi za Umma, Nyumba na Maendeleo ya Miji, na Bw. Anar Guliyev, Mwenyekiti wa Kamati ya Serikali ya Azerbaijan kuhusu Mpango wa Miji na Usanifu Majengo na Mratibu wa Kitaifa wa WUF13.

Mkataba huo wa Maelewano unaanzisha mfumo wa ushirikiano katika mpango jumuishi wa miji na maeneo, miji endelevu, mbinu za kisasa za maendeleo ya miji, mpango wa matumizi ya ardhi na ubadilishanaji wa maarifa. Unaendeleza pia ushirikiano katika miradi ya kimataifa ya maendeleo ya miji na unatoa fursa za ushirikiano wa kiufundi kati ya nchi hizo mbili. Ushirikiano wa Kenya na Azerbaijan unakuja wakati ambapo nchi zote mbili zinatekeleza mipango mikubwa ya mageuzi ya miji. Uzoefu wa Azerbaijan katika kujijenga upya baada ya mgogoro, maendeleo ya kisasa ya miji, mifumo endelevu ya usafiri na mageuzi ya mpango wa miji unatoa mafundisho muhimu kwa miji ya Kenya inayokua kwa kasi. Vilevile, Mpango wa Nyumba za Bei Nafuu wa Kenya, miradi ya ustahimilivu wa mabadiliko ya hali ya anga na mbinu bunifu za ufadhili zinatoa fursa za kujifunza pamoja na ushirikiano.

Kutiwa saini kwa Mkataba huo wa Maelewano kunaashiria sura mpya katika uhusiano wa Kenya na Azerbaijan na kunaonyesha umuhimu wa ushirikiano wa kimataifa katika kushughulikia changamoto za nyumba na kuendeleza miji endelevu. Kupitia ushirikiano huu, nchi zote mbili zinatarajiwa kuimarisha zaidi ubadilishanaji wa maarifa ya kiufundi, kuimarisha uwezo wa kitaasisi na kuendeleza masuluhisho bunifu yanayochangia miji jumuishi, thabiti na ya kudumu.